## Maswali

1. Mbona Mungu alituma gharika?
2. Wakati huo nani pekee yake alikuwa haki?
3. Mungu alimwambia Nuhu afanye nini?
4. Nuhu aliwambia watu watubu. Walimsikiliza?
5. Watu wangapi walienda kwa safina?
6. Nini ingine iliingia kwa safina?
7. Mvua ilinyesha kwa mda gani?
8. Nini ilifanyika kwa watu waovu?
9. Nuhu alifanya nini alipotoka kwa safina?
10. Mungu aliahidi nini? Alipeana ishara gani?

## Majibu

1. Kwa sababu watu wote walikuwa waovu.
2. Nuhu.
3. Ajenge safina.
4. Hapana.
5. 8
6. Wawili wa kila aina ya wanyama.
7. Usiku 40 na mchana 40.
8. Wote walizama.
9. Nuhu alishukuru Mungu na akamtolea sadaka kwa madhabahu.
10. Mungu aliahidi kwamba hataharibu nchi tena kwa gharika. Alipeana upinde kama ishara ya agano.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

## Awamu ya 2    Mwaka wa 1

# 3    Nuhu

**Kwa Biblia** Mwanzo 6:1-8 na 13-22; 7:1-12; 8:4-22; 9:12-15


### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu hapendi uovu. Nuhu alitii kikamilifu maagizo ya Mungu. Mungu huokoa wamwaminio

### Somo


Somo hili la Nuhu lilikuweko karibu miaka elfu moja baada ya Adamu na Hawa kumzaa Sethi. Kwa mda mrefu huo, watu wengi walikuwa wameongezeka duniani. Watu walikuwa wamesahau Mungu na kuwa waovu. Mungu alikuwa na uchungu na kusikitika kwa kuwaumba watu hawa. Aliamua kuwaua watu hawa waovu kwa gharika kubwa. Mungu alichunguza watu wa dunia wote na kupata familia moja tu ndio ilimpendeza. Nuhu na familia yake walikuwa haki na walimpenda Mungu.

Mungu alimwambia Nuhu kwamba ataleta gharika itakayoharibu watu wote. Mungu aliambia Nuhu ajenge safina kubwa. Nuhu na familia yake watakuwa salama gharika itakapo kuja. Mungu alimwelezea Nuhu vile safina itatengenezwa. Ilitengenezwa kwa mbao ngumu itwayo mvinje. Ilipakwa lami nje na ndani ili maji yasingie. Safina ilikuwa na orofa tatu na ikagawanywa kwa sehemu. Ilikuwa na mlango na dirisha. Nuhu aliamini kwamba Mungu alimwamini sawasawa. Nuhu pamoja na wanawe, kwa miaka mingi walifanya bidii kwa kujenga safina. Walitumia vifaa kama mawe au mivupa hata labda vyuma.



Nuhu alihadharisha watu kwamba Mungu ataleta gharika kubwa na itaharibu dunia yote. Aliambia watu watubu na kumrudia Mungu. Lakini watu hawakumsikiliza. Walimcheka alipokuwa akijenga hiyo safina kubwa mbali na bahari. Nuhu alimwamini Mungu na akaendelea kujenga safina kwa bidii akitumia maagizo yake.

Mwishowe safina ilimalizika. Mungu alileteа Nuhu kila aina ya wanyama – mme na mke. Mungu alimletea aina saba ya wanyama wanaoliwa. Wanyama wote waliingia kwa safina. Nuhu alichukuwa chakula cha kutosha wanyama wote. Aliingia kwa safina na mkewe, wana wao watatu na wake wao – watu wanane. Nuhu alikuwa na miaka 600 alipoingia kwa safina. Baada ya Nuhu na familia yake kuingia safinani, Mungu alifunga mlango.



Baada ya Nuhu na familia yake kuingia kwenye safina salama salamini, Mungu alileta gharika kubwa mno kwa nchi nzima. Mvua ilinyesha, bahari na mito zikavurika na kukawa na mawimbi makubwa. Kulikuwa na gharika pia. Watu waliogopa. Maji yalikuwa kila pahali. Watu waliskitika na kujilaumu wenyewe na kusema kama tungemsikia Nuhu! Lakini haikuwezekana! Bunde tu, watu wote walifunikwa kwa maji.

Mvua ilinyesha kwa siku arobaini. Maji yalivurika mpaka nchi na hata milima mirefu ikafunikwa. Nuhu alikuwa ndani ya safina kwa mwaka moja na siku kumi kwa sababu maji yalikauka baada ya miezi 11.

Baada ya miezi 5, safina ilitua juu ya milima mirefu iitwayo Ararati. Baada ya miezi mingine 3 Nuhu angeona juu ya milima. Akaongoja siku 40 tena. Akatuma kunguru. Lakini kunguru hakupata pahali pakutua ili apumzike. Baadaye Nuhu alituma njiwa ikaenda na kurudi. Akakaa siku saba na akatuma njiwa tena. Wakati huu njiwa ilirudi na jani la mzeituni mdomoni. Nuhu akajua kwamba maji yameenda chini ya miti.

Baada ya miezi 11, Nuhu alifungua sehemu ndogo kwa paa na akaangalia nje. Akaona ardhi imekauka. Baada ya mwezi moja, Mungu alimwambia Nuhu atoke nje ya safina.

Nuhu pamoja na familia yake na wanyama walitoka nje ya safina. Walikuwa wamekaa kizani mwa safina kwa zaidi ya mwaka moja. Walitoka nje kwa ulimwengu mpya. Kila kitu na kila mtu waliowajua waliharibiwa. Nuhu na familia yake walibaki kuanza maisha mapya.

Nuhu alishukuru Mungu kwa kumuokoa kutoka kwa gharika. Alijenga madhabahu ili amtolee Mungu sadaka ya shukrani. Alisifu Mungu kwa kumuokoa yeye na familia yake.

Mungu alimbariki Nuhu na familia yake. Aliwambia wawe na watoto wengi kuanzisha uzao mpya utakaopenda na kumwabudu Mungu. Mungu alimpa Nuhu ahadi ya kipekee. Alimwambia kwamba hataharibu ulimwengu tena kwa kutumia gharika. Aliweka upinde mzuri juu angani kama ishara ya hiyo agano. Tunapoona upinde tunakumbuka ahadi ya Mungu.

